JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

---

# TAARIFA KWA UMMA
## KUHUSU KUSITISHA UCHAGUZI KATIKA JIMBO LA SIHA WILAYA YA SIHA MKOA WA KILIMANJARO

**Tarehe 08 Oktoba, 2025**

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 71(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 na kwa barua ya tarehe 08 Oktoba, 2025 isiyokuwa na Kumbukumbu Namba kutoka kwa Katibu wa Chama cha Wananchi CUF Wilaya ya Siha nimepokea taarifa ya kifo cha Ndugu Daudi Wilibrod Ntuyehabi aliyekuwa mgombea wa nafasi ya Ubunge Jimbo la Siha Wilaya ya Siha kupitia Chama cha Wananchi CUF.

Kutokana na kutokea kwa tukio hilo, Uchaguzi wa Ubunge katika Jimbo la Siha, Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro umesitishwa kuanzia leo tarehe 08 Oktoba, 2025. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 71 (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali itapanga tarehe nyingine ya uteuzi wa wagombea na taratibu za uchaguzi wa Ubunge katika jimbo husika zitaanza upya.

Hivyo, uteuzi kwa wagombea wengine ambao walioteuliwa kihalali utabaki kama ulivyokuwa awali, isipokuwa kama mgombea atajitoa na kwamba hakutakuwa na kampeni kwa wagombea Ubunge katika jimbo la Siha mpaka baada ya uteuzi wa mgombea mwingine.

***"KURA YAKO HAKI YAKO JITOKEZE KUPIGA KURA"***

Imetolewa na:

Marco F. Masue
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**
**JIMBO LA SIHA**
**WILAYA YA SIHA**

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA SIHA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA

UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura